

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Kingalu  
S.L.P 845 MOROGORO  
Simu: 023-2614302  
Nukushi: 023-2614478  
Barua Pepe: [rbcmorogoro@pccb.go.tz](mailto:rbcmorogoro@pccb.go.tz)  
Wavuti: [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI**

---

Juni 10, 2020

**DIWANI NA WATAALAM WA ARDHI MAHAKAMANI KWA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro inapenda kuwajulisha Umma kwamba kwamba leo Jumatano - Juni 10, 2020 itawafikisha Mahakamani Diwani ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa Morogoro **Amir Juma Nondo** pamoja na waatalam wa ardhi kujibu mashtaka yanayowakabili.

Pamoja na Diwani huyo watashtakiwa wengine ni **Simon Michael Mahundo** aliyekuwa Afisa Mipangomiji, **Athumani Leonard Juma** aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Mipangomiji na Mazingira wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na **Dickson Steven Kesenha** ambaye alikuwa ni Afisa Mipangomiji wa ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro ambapo wote kwa pamoja wanakabiliwa na makosa yafuatayo;

- i. Matumizi ya nyaraka kumdanganya mwajiri
- ii. Kushiriki kutenda uovu
- iii. Matumizi mabaya ya mamlaka
- iv. Kuwasilisha nyaraka za uongo
- v. Kughushi

Watumiwa hawa watafikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro majira ya saa 5 Asubuhi.

Imetolewa na:

Janeth Machulya  
**Mkuu wa TAKUKURU (M)**  
**MOROGORO**